JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA

# TAARIFA YA UKAGUZI WA DAWA, VIFAA TIBA NA VITENDANISHI KATIKA SOKO NA MAENEO YA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA 2021/2022

KANDA YA MASHARIKI

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba, TMDA Kanda ya Mashariki
P. O. Box 31356, Jengo la Victoria, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, Dar es Salaam
Tel: +255-737-226328/788470301, Fax: +255-22-2450793
Website: www.tmda.go.tz, Email: info.eastzone@tfda.go.tz

## 1.0. UTANGULIZI

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ina jukumu la kulinda afya ya jamii kwa kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

Taarifa hii inaonesha utekelezaji wa kazi za ukaguzi kwa Ofisi ya Kanda ya Mashariki kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22 ambazo zilizingatia mpango kazi na misingi ya vihatarishi ambavyo vingeweza kuwa vichocheo vya ukiukwaji wa Sheria.

## 2.0 LENGO LA KAGUZI ZILIZOFANYIKA

Kaguzi zililenga kufuatilia ubora wa bidhaa za dawa (binadamu na mifugo), vifaa tiba na vitendanishi vilivyopo katika soko (maduka na maghala) pamoja na vinavyotumika katika vituo vya kutolea huduma za afya (hospitali, vituo vya afya, zahanati na maabara) kwa kuhakiki utekelezaji wa Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba Sura 219 kwa;

2.1 Kubaini uwepo wa bidhaa za dawa, chanjo, vifaa tiba na vitendanishi ambazo hazijasajiliwa.

2.2 Kubaini uwepo wa bidhaa za dawa, chanjo, vifaa tiba au vitendanishi zenye ubora duni.

2.3 Kubaini uwepo wa bidhaa za dawa, chanjo, vifaa tiba na vitendanishi ambazo ni bandia.

2.4 Kuhakiki utekelezaji wa Kanuni ya *The Tanzania Food, Drugs and Cosmetics (Recall, Handling and Disposal of Unfit Medicines And Cosmetics) Regulations, 2015* ambayo inahusu uondoaji, utunzaji na uteketezaji wa bidhaa dawa, chanjo, vifaa tiba na vitendanishi zisizofaa kwa matumizi.

2.5 Kuhakiki ubora wa majengo na mazingira ya uzalishaji, usambazaji, uhifadhi na uuzaji.

## 3.0 UKAGUZI KATIKA SOKO NA MAENEO YA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22, Kanda ya Mashariki ilikagua jumla ya maeneo **2,274** katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga ambapo famasi za dawa za binadamu **521**, maghala ya dawa **163**, viwanda **31**, maduka ya dawa muhimu (DLDM) **806**, maduka ya dawa za mifugo **356**, maduka ya vifaa tiba **57**, maghala ya vifaa tiba **24,** maduka ya kawaida (*general sales*) **14,** hospitali **78**, kliniki za kibingwa (*polyclinics*) **40**, zahanati **133** na maabara **51.**

Hatua mbalimbali zilichukuliwa kwa maeneo ambayo hayakukidhi matakwa ya Sheria ikiwa ni pamoja na kuondoa bidhaa zilizobainika kuwa na ubora duni na ambazo hazijasajiliwa, kutoa muda wa kufanya marekebisho ya majengo yaliyokuwa na mapungufu, kutoza **25%** ya thamani ya bidhaa zilizoondolewa ambayo ni

gharama ya uteketezaji. Mchanganuo wa majengo na maeneo yote yaliyokaguliwa umeainishwa katika majedwali hapo chini;

**Jedwali Na. 1: Ukaguzi wa maeneo ya biashara ya dawa na vifaa tiba**

| Mkoa | Famasi | Maghala za (Dawa binadamu) | Viwanda | Maduka ya dawa za mifugo | DLDM (Dawa za binadamu) | Maduka ya Vifaa Tiba | Maghala (Vifaa Tiba) | Maduka ya Bidhaa za Kawaida (*General* | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 429 | 161 | 25 | 220 | 469 | 54 | 18 | 14 | **1,390** |
| Tanga | 28 | - | - | 106 | 189 | - | - | - | **323** |
| Pwani | 64 | 2 | 6 | 30 | 148 | 3 | 6 | - | **259** |
| **Jumla** | **521** | **163** | **31** | **356** | **806** | **57** | **24** | **14** | **1,972** |

**Jedwali Na. 2: Ukaguzi wa vituo vya kutolea huduma za afya**

| Mkoa | Hospitali | Kliniki za kibingwa (*polyclinics*) | Zahanati | Maabara | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 54 | 32 | 46 | 45 | **177** |
| Tanga | 11 | - | 39 | - | **50** |
| Pwani | 13 | 8 | 48 | 6 | **75** |
| **Jumla** | **78** | **40** | **133** | **51** | **302** |

## 4.0 UTEKETEZAJI WA BIDHAA ZISIZOKIDHI VIWANGO

Jumla ya tani **394.39** za bidhaa zisizokidhi viwango zenye thamani ya **TZS: 8,944,671,898.40** ziliteketezwa kwa hiari. Aidha, bidhaa za dawa na vifaa tiba zenye thamani ya **TZS: 56,876,886.40** zilizokamatwa zinategemea kuteketezwa katika mwaka wa fedha 2022/23. Mchanganuo wa bidhaa zilizoteketezwa ni kama ulivyoainishwa kwenye jedwali hapo chini:

**Jedwali Na. 3: Uteketezaji wa bidhaa zisizokidhi viwango zilizotolewa taarifa**

| Na. | Aina ya bidhaa | Uzito (MT) | Thamani (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1. | Dawa | 261.39 | 6,848,629,888.00 |
| 2. | Vifaa tiba na Vitendanishi | 133 | 2,096,042,010.40 |
| **Jumla** | | **394.39** | **8,944,671,898.40** |

## 5.0 CHANGAMOTO

Changamoto zilizojitokeza ni pamoja na;

5.1 Baadhi ya wafanyabiashara kuingiza nchini bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi ambazo hazijasajiliwa, zenye ubora duni au bandia kwa njia za kificho au kupitia mipaka isiyo rasmi.

5.2 Baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kufanya biashara ya bidhaa za dawa, vifaa tiba au vitendanishi bila kuzingatia sheria, taratibu na kanuni zilizopo.

## 6.0 MAFANIKIO

6.1 Kuongezeka kwa utii wa sheria bila shuruti *(voluntary compliance)* kwa wafanyabiashara wa bidhaa zinazodhibitiwa na TMDA. Hii imedhihirika kwa wateja kutoa taarifa bidhaa zinapokuwa zimeisha muda wake wa matumizi kwa ajili ya uteketezaji pamoja na kuripoti ili ziteketezwe.

6.2 Kuongeza idadi ya wakaguzi wapya kupitia mafunzo yaliyotolewa kwa wakaguzi wa Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam ambapo jumla ya wakaguzi **35** walipata mafunzo hayo.

6.3 Wakaguzi kupata mafunzo ya mara kwa mara juu ya mifumo ya ubora na udhibiti wa vihatarisho.

## 7.0 HITIMISHO

TMDA Kanda ya Mashariki inatoa shukrani za dhati kwa ushirikiano ambao imekuwa ikiupata kutoka kwa wadau mbalimbali ikiwemo viongozi na watendaji katika sekta za umma na binafsi katika kufanikisha utekelezaji wa kazi za ukaguzi.

**IMEANDALIWA NA TMDA KANDA YA MASHARIKI**

**A. A. BITEGEKO**
**MENEJA WA KANDA**